# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA





## ZIARA ZA KAMATI ZA KUDUMU ROBO YA PILI MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### OKTOBA-DISEMBA

Kila robo ya mwaka wa fedha kamati za kudumu za Halmashauri hukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kujionea shughuli zinavyotekelezwa, thamani ya fedha iwapo inaendana na miradi hiyo, kushauri na kubaini changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi.

Katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/20223 ambayo huanza mwezi Oktoba hadi Disemba, Kamati hizo za Kudumu ambazo ni Kamati ya UKIMWI, Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu, Kamati ya Mipangomiji, Ujenzi na Mazingira, Kamati ya Fedha na Uongozi zimekagua miradi katika sekta ya Afya, Elimu, vyanzo cha mapato, kufuatilia masuala ya mazingira, pamoja na miradi ya ardhi.



*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

### YALIYOMO


Ukurasa wa 2:
Ziara Kamati ya Menejimenti





Ukurasa wa 3:
Ziara Kamati ya UKIMWI





Ukurasa wa 4:
Ziara Kamati ya Huduma





Ukurasa wa 5:
Ziara Kamati ya Mipangomiji





Ukurasa wa 6:
Ziara Kamati ya Fedha






24 JANUARI 2023

# ZIARA YA KAMATI YA MENEJIMENTI











*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023 inayoanza Oktoba na kukamilika mwezi Disemba, Kamati ya Menejimenti ilikagua miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na fedha za mapato ya ndani pamoja na miradi ambayo inahusika moja kwa moja na mapato ya ndani

Miradi ambayo ilikaguliwa ni pamoja na maendeleo ya ujenzi wa shule ya Msingi Shibula, Shule ya Msingi Kahama, ukarabati wa mzani katika mwalo wa samaki, ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha Afya Buzuruga , umaliziaji wa maabara katika shule ya sekondari Buzuruga, stendi ya mabasi ya nyamhongolo pamoja na jengo la utawala ambalo lipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Katika ziara hiyo wajumbe walishauri kuwa miradi hiyo ikamilike kwa wakati ili iweze kuanza kutumika kuweza kutimiza malengo tarajiwa ambayo ni kuboresha huduma kwa wananchi pamoja na hayo walishauri katika miundombinu iliyojengwa kuwepo na miundombini kwa ajili ya walemavu



15 FEBRUARI,2023

# ZIARA YA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI











*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Katika ziara hii ya kamati ya Kudhibiti UKIMWI wataalam wa afya walishauriwa kutokukata tamaa katika kuwahudumia watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa upungufu wa kinga mwilini maarufu UKIMWI

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya UKIMWI ya manispaa ya Ilemela Mhe Manusura Lusigaliye wakati hii kwa ajili ya kufuatilia shughuli zinazotekelezwa juu ya kudhibiti na kupambana na maambukizi ya ugonjwa huko katika vituo vya afya vya Buzuruga na Pasiansi.

Pamoja na hilo wajumbe waliwapongeza kwa namna wanavyotoa huduma kwa wananchi pamoja na jitihada wanazochukua katika kukabiliana na maambukizi mapya huku akiwasisitiza kuendelea kutoa elimu kwa baadhi ya wateja wao wasiokuwa waaminifu wanaobadili majina wakati wa kupata huduma na wale wanaotoroka

Sambamba na hilo Mhe Manusura ameahidi kuzifanyia kazi changamoto zote zilizobainishwa na watoa huduma za afya wakati wa ziara hiyo, huku Mhe Sara Ng'wani ambae ni mjumbe wa kamati aliwakumbusha wanaume kuwa mstari wa mbele katika kujua afya zao pamoja na kushirikiana na wenzao katika kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI

Kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba-Desemba Zahanati ya Pasiansi ina jumla ya wateja waliopo kwenye huduma 1308, wanaume 388, Wanawake 920 na watoto 21 wakati kituo cha afya Buzuruga kikiwa na jumla ya wateja 3180 wanaume 907 na Wanawake 2273.



16 FEBRUARI, 2023

# ZIARA YA KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI,AFYA NA ELIMU











*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Wananchi wa wilaya ya Ilemela wamepongezwa kwa namna wanavyoshiriki na kuchangia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta mbalimbali hususan afya na elimu.

Pongezi hizo zimetolewa na kamati ya huduma za uchumi, elimu na afya chini ya Mwenyekiti wake Mhe Andrea Nginila wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo ameridhishwa na namna wananchi walivyojitoa katika kuchangia nguvu na fedha kufanikisha ujenzi wa miradi mbalimbali.

Katika ziara hiyo kamati ilifanikiwa kutembelea miradi ya ujenzi wa maboma saba na ofisi mbili za shule mpya ya msingi shibula kata ya Shibula, ujenzi wa hosteli na maabara ya shule ya sekondari Igogwe kata ya Bugogwa na ujenzi wa jengo la nyumba ya watumishi zahanati mpya ya Mihama kata ya Kitangiri.




17 FEBRUARI, 2023

# ZIARA YA KAMATI YA MIPANGOMIJI, UJENZI NA MAZINGIRA












*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Wataalam wa ardhi wametakiwa kuepusha migogoro ya ardhi ambayo inaweza kuisababishia hasara Manispaa ya Ilemela.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya ardhi na mipangomiji wakati wa akihitimisha ziara ya kamati hiyo ya robo ya pili kipindi cha Oktoba-Disemba mwaka wa fedha 2022/2023

Pamoja na hayo rai imetolewa kwa wananchi kuhakikisha kuwa wanafuata taratibu zote za mipangomiji ikiwa ni pamoja kuhakikisha kuwa kabla ya kuanza ujenzi wanapata kibali cha ujenzi ili kuepukana na kubomolewa nyumba zao.

Kamati hiyo ya mipangomiji ilifanya ziara kwa lengo ikiwa ni kukagua ujenzi unaoendelea katika kata za Manispaa ya Ilemela kwa ajili ya kukagua vibali vya ujenzi pamoja na kuona kama taratibu zote zimefuatwa, pamoja na kufanya utatuzi wa migogoro ya ardhi inayoendelea.

Katika ziara hiyo wajumbe kwa kauli moja walizuia ujenzi uliokuwa ukiendelea katka eneo la Buyombe pamoja na ujenzi eneo la kata ya Kiseke kutokana na kuwa wahusika wa maeneo hayo walikiuka taratibu za ujenzi.



21 Februari, 2023

# ZIARA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI











*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Watalaam wa Ilemela watakiwa kuweka mkazo katika suala la ukusanyaji wa mapato, ili kuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato katika bajeti inayoendelea ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Hiyo ni rai iliyotolewa na wajumbe wa kamati ya Fedha na uongozi wakati wa kuhitimisha ziara ya kamati ya fedha kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba –Disemba 2022/2023 ambapo kamati hii inalo jukumu kubwa la kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

Katika ziara hiyo ambayo ililenga kukagua masoko ya Ilemela ikiwa ni moja ya chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na vyanzo vingine wajumbe walishauri uboreshaji mbalimbali katika vyanzo hivyo ili kuweza kuweka mazingira bora kwa watumiaji.

Kamati ya fedha kwa robo ya pili ilikagua soko la magomeni, Nyasaka, Soko la mbao nyakato, stendi ya Nyamhongolo , stendi ya Buzuruga na mzani wa mazao ya uvuvi wa mwaloni vyote hivi vikiwa ni vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri.